- Kanuni zimeongeza fomu mpya zinazohusiana na taarifa ya nia ya kukata rufaa ambazo zinaweza kuwasilishwa na mrufani ambaye yuko gerezani; fomu hizi ni B/1 na C/1.

- Orodha ya kesi za mamlaka ambazo mrufani/mrufaniwa anataka kuzitumia wakati wa kusilikilizwa kwa rufaa lazima ziwasilishwe mahakamani zikiwa katika nakala nane.

- Kwa taarifa ya ziada ya rufaa, mhusika katika rufaa anatakiwa kuwasilisha katika masjala inayohusika nakala nane za taarifa ya rufaa ya ziada ikiambatana na kesi za mamlaka na hati zingine ambazo atazitumia katika rufaa.

- Mhusika katika rufaa anaweza kumwandikia Msajili moja kwa moja kama anataka kubadilisha wakili badala ya wakili wake kumwandikia Msajili kumfahamisha nia ya kujitoa katika kesi.

- Kanuni mpya pia zinaruhusu matumizi ya Sheria ya Mwenendo wa Madai katika utaratibu wa kuwasilisha wito kwa wahusika katika rufaa.

- Kanuni mpya zinatoa haki ya ujumla kwa Mahakama kuongeza muda wa rufaa/maombi bila kujali aina ya maombi.

Imeandaliwa na:

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

Jengo la Haki

Mtaa wa Luthuli

S.L.P. 3580

Simu: +255 22 211387/2123533

Nukshi: +255 22 2123534

Barua pepe: lrct@lrct.or.tz

© LRCT 2010

KWA UDHAMINI WA PROGRAM YA KUIMARISHA MAZINGIRA YA BIASHARA TANZANIA (BEST)

Printed By Rainbow Printers, Email: info@rainbowprinters.co.tz

PROGRAM YA KUIMARISHA MAZINGIRA YA BIASHARA TANZANIA

(BEST)

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MAHAKAMA YA RUFAA TANZANIA ZA 1979

Wakati usuluhishi wa migogoro ya biashara unaposhindikana, wahusika wa migogoro hiyo hawana njia nyingine zaidi ya kufungua shauri la madai Mahakamani. Mahakama ya juu kabisa katika kusikiliza mashauri ni Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Pamoja na matumizi ya sheria nyingine, kanuni zinazotumika katika Mahakama hii ni Kanuni za Mahakama ya Rufaa.

Kanuni za Mahakama ya Rufaa ziliundwa mwaka 1979 na zimekuwa zikitumika toka wakati huo katika utaratibu wa kuendesha rufaa katika ngazi ya Mahakama ya Rufaa. Kutokana na mabadiliko ya kijamii pamoja, kanuni hizi zimekuwa haziendani na wakati na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa kusikiliza kesi Mahakamani.

Kwa kupitia Program ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST) chini ya eneo la Utatuzi wa Migogoro ya Biashara, Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania Augustino Ramadhani aliielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kuzipitia na kuzifanyia marekebisho Kanuni za Mahakama ya Rufaa za 1979. Maelekezo haya yalikuja baada ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kuandaa Waraka wa Majumuisho (position paper) wa mwaka 2006 ambao ulihusu Mapitio ya Mfumo wa Madai Tanzania (Civil Justice Review).

Tume inatambua mchango mkubwa wa Dkt. Angelo Mapunda wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyezifanyia kazi Kanuni hizi kuanzia maandalizi ya Waraka wa Majumuisho ya Awali kuhusu Kanuni za Mahakama ya Rufaa za 1979 taarifa iliyoonyeshwa matatizo yaliyokuwepo kwenye Kanuni hizi za Mahakama ya Rufaa pamoja na Sheria ya Mahakama ya Rufaa ya 1979.

Tume iliutumia waraka uliondaliwa na Dkt. Angelo Mapunda katika kutafuta maoni na mapendekezo ya kuziboresha Kanuni hizi kutoka kwa wadau mbalimbali na taarifa ya maoni na mapendekezo hayo iliwasilishwa kwa Kamati ya Kanuni hizi iliyokuwa inaongozwa na Jaji Nsekela wa Mahakama ya Rufaa.

Wadau mbalimbali walihusishwa katika kuzipitia Kanuni za Mahakama ya Rufaa ili kuweza kutoa maoni na mapendekezo ya kuziboresha. Mikutano mbalimbali ilifanyika ili kupata maoni na mapendekezo kuhusu Kanuni hizi kupitia Waraka huo. Mikutano hii ilifanyika kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, 2008 na ilihusha wadau wafuatao: Mawakili wa Tanzania Bara, Mawakili wa Serikali, Waadhiri kutoka Vitivo vya Sheria na Chuo Kikuu cha Polisi, Maafisa Sheria wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania pamoja na Asasi zisizo za Kiserikali ambazo zinatoa msaada wa sheria. Majaji wa Mahakama Kuu wa Tanzania Bara na Zanzibar walikutana tarehe 11 Oktoba, 2008. Mawakili wa Kujitegemea na Mawakili wa Serikali Zanzibar walikutana tarehe 24 Oktoba, 2008, Majaji wa Mahakama ya Rufaa Tanzania walikutana kwa siku tatu kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 17 Desemba, 2008 na mwisho Kamati ya Majaji wanne wa Mahakama ya Rufaa wakiwemo Jaji Nsekela, Jaji Rutakangwa, Jaji Kimaro na Dkt Bwana wakiongozwa na Jaji Nsekela walikutana kwa siku mbili kwa ajili ya kufanya majumuisho na kukamilisha taarifa kamili ya mapendekezo ya marekebisho, ambayo yaliwasilishwa kwa Jaji Mkuu.

Kanuni mpya za Mahakama ya Rufaa za 2009 zilizosainiwa na Jaji Mkuu zilitolewa katika Gazeti la Serikali Na. 368 la Novemba 2009 na Kanuni hizi zimeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 01.02.2010 kwa mujibu wa Gazeti la Serikali Na. 36 la 2010. Yafuatayo ni mabadiliko ambayo yameletwa na Kanuni mpya za Mahakama ya Rufaa.

- Kanuni zimeondoa taratibu za kiufundi na sasa zinazingatia utoaji wa haki kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano.

- Kuongeza muda katika shauri kwa hali yoyote kutawezeshwa na sababu nzuri na si kwa kuonyesha sababu inayotosheleza.

- Kanuni zimeweka ulazima wa kuwasilisha Mahakamani majumuisho ya maandishi ndani ya siku 60 baada ya kuwasilisha rufaa mahakamani.

- Kanuni zimeongeza muda wa kuwasilisha mahakamani taarifa ya nia ya kukata rufaa, kutoka siku 14 hadi siku 30 na taarifa hii kuwasilishwa kwa upande mwingine ndani ya siku 14 badala ya siku 7 kama ilivyokuwa hapo awali.

- Taarifa ya pingamizi la awali lazima iwasilishwe Mahakamani siku tatu kabla ya tarehe ya kusikilizwa rufaa na lazima taarifa hii iwe katika nakala tano ambazo zitawasilishwa kwa Msajili.